

13.3.5:TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA NYUMBA BORA YA MWANANCHI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDUGU CHARLES FRANCIS KABEHO TAREHE 05-06-2018

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, ninayo furaha kubwa sana kukukaribisha wewe pamoja na msafara wako wote uliofuatana nao hapa Kijiji cha Kagugu, nasema karibu sana.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, mradi huu wa ujenzi wa nyumba bora niliufikiria baada ya kuona watu wengi wanakimbilia kujenga nyumba bora Mijini. Hivyo mimi niliamua kujenga nyumba hii hapa Kijijini ili jamii ifahamu kuwa hata Vijijini tunatakiwa kuishi kwenye nyumba bora.

Ndugu, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, ujenzi wa nyumba hii ulianza mwaka 2017 na kukamilika Mwaka huu. Hivyo kufanya gharama ya ujenzi wa nyumba hii hadi sasa kuwa Tshs. **70,000,000/=**.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Nyumba hii ina vyumba vitatu vya kulala, Sebule,Jiko,sehemu ya kulia na stoo. Nyumba hii imekua kama kivutio na ina hamasisha Wanakijiji kuhusu ujengaji wa nyumba bora.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, Wazazi wangu waliwekeza kwenye elimu yangu ndio maana leo nimeweza kujenga nyumba bora hapa Kijijini kwetu .Hivyo naungana na kauli mbiu isemayo **“Elimu ni ufunguo wa maisha,Wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu”**.

Ndugu, Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2018, baada ya taarifa hii fupi kwa Heshima na Taadhima nakuomba sasa unifungulie nyumba yangu.

Kwa niaba ya,

Dr Pasishesh Mapunda
**MWANANCHI
KIJIJI CHA MBANGAMAO**